



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

# News Bulletin



[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)



Wizara ya Nishati



wizara\_ya\_nishati\_tanzania



@Nishati2017



Wizara ya Nishati

Toleo Namba 47

Februari 1 - 28, 2023

## MFUKO WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA WAKABIDHI SH. BILIONI 3.21 KWA WASAMBAZAJI GESI YA MITUNGI



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akitabidhi hundi kwa mmoja wa wanufaika wa ruzuku ya Shilingi bilioni 3.21 iliyotolewa na Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) Tanzania kwa kampuni 16 zinazojishughulisha na utoaji wa huduma za uuzaji wa nishati safi ya kupikia nchini. Hafla hiyo ilifanyika mkoani Dar es Salaam.



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma



## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
**Mhandisi Felchesmi Mramba**  
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**  
Kheri Mahimbali

**Mhariri**  
Dorina G. Makaya

**Waandishi**  
Teresa Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar  
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**  
Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu  
namba +255-26-2322018  
Nukushi: +255-26-2320148  
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma




[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

[Wizara ya Nishati](#)


[@Nishati2017](#)

[wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)



# MFUKO WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA (COOKFUND) WAKABIDHI RUZUKU YA SHILINGI BILIONI 3.21 KWA WASAMBAZAJI WA GESI YA MITUNGI



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akikabidhi hundi kwa baadhi ya wanufaika wa ruzuku ya Shilingi bilioni 3.21 iliyotolewa na Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) Tanzania kwa kampuni 16 zinazojishughulisha na utoaji wa huduma za uuzaaji wa nishati safi ya kupikia nchini. Hafla hiyo ilifanyika mkoani Dar es Salaam.

**M**fuko wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) Tanzania imetoa ruzuku yenye thamani ya Shilingi Bilioni 3.2 kwa kampuni 16 zinazojishughulisha na utoaji wa huduma za uuzaaji wa nishati safi ya kupikia nchini kwa lengo la kuzisaidia kutoa huduma hizo kwa gharama nafuu na zenye ubora unaowanufaisha wateja wa kipato cha chini nchini Tanzania.

Wanufaika hao 16 ni mtokeo ya mwito wa kwanza wa maombi ya ufadhili yaliyotolewa mnamo Septemba 2022 kupitia programu hiyo inayofadhiliwa na Umoja

wa Ulaya (EU) ukilenga katika maeneo ya teknolojia safi ya kupikia hususani gesi ya 'mitungi' yaani Liquified Petroleum Gas (LPG), majiko ya umeme (EPC), majiko ya mkaa banifu (ICS) mkaa tofali utokanao na vumbi la makaa ya mawe (briquettes) na nishati ya mafuta itokanayo na mabaki ya mimea (bioethanol).

Hafla fupi ya kukabidhi hundi za fedha kwa wanufaika hao ilifanyika mkoani Dar es Salaam ikiongozwa na Waziri wa Nishati, January Makamba sambamba na Balozi wa Umoja wa Ulaya, Manfredo Fanti, na Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa

Umoja wa Mataifa (UNCDF) Tanzania Peter Malika ambaye mfuko wake ndio unaratibu programu ya CookFund.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Waziri Makamba aliwasisitiza wanufaika wa ruzuku hiyo kuhakikisha wanazitumia fedha hizo kulingana na malengo ya mpango huo ili mtokeo mazuri ya mpango huo yaweze kuwafikia Watanzania wengi.

"Ni vyema mkafahamu kuwa huu si mkopo bali ni ruzuku ambayo mnaipata moja kwa moja kwa jina la nchi yetu. Hivyo ni vyema mkahakikisha Watanzania wanufaika kweli kupitia mpango huu kwa

kuwafikishia bidhaa zenu za nishati kwa bei nafuu ili waweze kuondokana na matumizi ya nishati chafu ambazo si rafiki kwa mazingira," alisema

Akizungumzia zaidi programu ya CookFund Waziri Makamba alisema ni moja ya suluhu la msingi kwa nchi katika kupambana na matumizi ya nishati chafu kwa sababu inawahakikishia wananchi upatikanaji wa nishati safi kwa gharama nafuu.

Kwa upande wake Balozi Manfred Fanti aliwataka wafanyabiashara walionufaika na ruzuku hiyo kuonyesha kwamba wanaweza kuuza bidhaa zao za nishati ya kupikia

# MFUKO WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA (COOKFUND)

## WAKABIDHI RUZUKU YA SHILINGI BILIONI 3.21

### KWA WASAMBAZAJI WA GESI YA MITUNGI

kwa bei nafuu na kwa wateja wengi wapya kupitia msaada wa kifedha walioupata kupitia mpango huo

"Umoja wa Ulaya (EU) unatarajia ruzuku hizi zitasaidia watumiaji wapya wa nishati ya kupikia hapa nchini kuweza kupata vifaa vyote vinavyohusika na mfumo mzima wa zana za kupikia kwa bei nafuu na zaidi tuendelea kuhamasisha watanzania wengi zaidi waendelee kuachana na mbinu za kupikia ambazo zinachafua na kuharibu mazingira".

"Tunatumai kushuhudia matokeo ya kuridhisha katika siku zijazo na kupungua kwa familia zinazotumia nishati ya kuni au mkaa kwa kupikia." Alisema.

Akitoa shukurani zake kwa Serikali ya Tanzania na Umoja wa Ulaya, Bw. Peter Malika alisema kwa kuzingatia athari kubwa ya matumizi ya nishati itokanayo na mimea katika suala zima la mapishi nchini, ipo haja ya msingi ya kuongeza uwekezaji katika mnyororo wa thamani kwenye

nishati safi ya kupikia ili kuharakisha mabadiliko kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Kwa kuwa hii ni awamu ya kwanza ya maombi yaliyoidhinishwa ambayo yanahusisha wanufaika 16 ambaao kwa jumla watahudumia kaya 191,336 katika maeneo yao na kutoa ajira 191 katika kipindi cha miaka mitatu, tunatarajia kuzindua mwito mpya wa mapendekezo mwezi huu kwa hivyo kuendelea awamu nydingine ya ruzuku kwa kama hizi," alibainisha.

CookFund ni programu ya miaka mitatu inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) chini ya Mpango wa mkakati jumuishi wa kutumia nishati safi ya kupikia nchini na Mfuko wa 11 wa Maendeleo ya Ulaya (EDF), unaolenga kuchangia dhamira ya Tanzania ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza sehemu ya idadi ya watu na upatikanaji endelevu wa ufumbuzi wa kupikia.

UNCDF ndio taasisi msimamizi na mtekelezaji wa programu ya CookFund. Mpango huu unalenga kushughulikia "upungufu wa mitaji" kwa upande wa watendaji wa sekta binafsi na changamoto ya kumudu gharama kwa watumiaji wa mwisho kwenye kaya.



Programu ya CookFund inachangia vipaumbele vyta kimkakati vyta Mfumo wa Ushirikiano wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania kwa kusaidia upatikanaji bora wa nishati safi na teknolojia, usimamizi endelevu wa maliasili na kuongeza kasi ya kazi zenye heshima katika sekta rasmi.

Kutoka Wizara ya Nishati, Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga na wataalam mbalimbali.



Balozi wa Umoja wa Ulaya, Manfredo Fanti, akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi hundi za fedha kwa kampuni 16 zinazojishughulisha na utoaji wa huduma za uuzaji wa nishati safi ya kupikia nchini kwa lengo la kuzaidia kutoa huduma hizo kwa gharama nafuu na zenye ubora unaowanufaisha wateja wa kipato cha chini nchini Tanzania. Hafla hiyo ilifanyika mkoani Dar es Salaam.

## MFUKO WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA (COOKFUND) WAKABIDHI RUZUKU YA SHILINGI BILIONI 3.21 KWA WASAMBAZAJI WA GESI YA MITUNGI



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akikabidhi hundi kwa baadhi ya wanufaika wa ruzuku ya Shilingi bilioni 3.21 iliyotolewa na Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) Tanzania kwa kampuni 16 zinazojishughulisha na utoaji wa huduma za uuzaji wa nishati safi ya kupikia nchini. Hafla hiyo ilifanyika mkoani Dar es Salaam.

# MAKATIBU WAKUU WASTAAFU WAPONGEZA UTEKELEZAJI MRADI WA JNHPP



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akizungumza na waandishi wa Habari wakati wa ziara ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wastaifu waliofika kuona maendeleo ya ujenzi wa Bwawa la kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

## Na Timotheo Mathayo, Rufiji

**K**atibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Baraza la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mha. Zena Ahmed Said amepongeza utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao unaendelea vizuri ukiwemo ujenzi wa Tuta Kuu pamoja na njia za kupitisha maji.

Mha. Zena ametoa kauli hiyo Jumamosi Januari 21, 2023 wakati

alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu Wastaifu wa Wizara mbalimbali kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao utazalisha umeme wa kiasi cha megawati 2,115.

"Ni matumaini yetu ikifika mwezi Juni 2024 ujenzi wa huu mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Nyerere utakuwa umekamilika kwa sababu hadi sasa mradi umefikia asilimia 80.2 na utaondoa

changamoto ya upatikanaji wa umeme nchini," alisema Mha. Zena.

Aliishukuru Wizara ya Nishati kwa kuwalika kutembelea mradi huo na pia alipongeza wakandarasi, Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) na msimamizi wa mradi TECU ambayo ni kampuni ya Tanzania kwa kusimamia ujenzi.

Aidha, Mha. Zena aliishauri Wizara ya Nishati kuandaa kanzidata itakayosaidia kufahamu wafanyakazi wote waliohusika katika ujenzi wa mradi huo ili waweze kutumika maeneo mengine yenye miradi ya kimkakati.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema Makatibu Wakuu Wastaifu waliotembelea mradi huo baadhi yao walihusika katika maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi walipokuwa Wizara ya Nishati na Madini au Wizara nyingine za kisekta walizokwu

wakifanyia kazi.

Mhandisi Mramba amesema kila mmoja amechangia mafanikio ya mradi huo na amewapongeza Makatibu Wakuu Wastaifu kwa kukubali mwaliko wa Wizara ya Nishati kwa kufika eneo la mradi kuona maendeleo yaliyofikiwa.

Katibu Mkuu mstaifu wa Wizara ya Utumishi, Bw. George Yambesi ambaye pia ni Katibu wa Makatibu Wakuu Wastaifu amesema viongozi wastaifu wataendelea kuwa mabalozi wa Miradi inayotekelzwa na Serikali ikiwemo ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP.

Ziara hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati akiwemo Naibu Katibu Mkuu, Bw. Kheri Abdul Mahimbali, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga, Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu, Bw. Edward Ishengoma pamoja na watendaji wengine wa Wizara ya Nishati na TANESCO.

# MAKATIBU WAKUU WASTAAFU WAPONGEZA UTEKELEZAJI MRADI WA JNHPP



Katibu Mkuu Kiongozi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Baraza la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mha. Zena Ahmed Said (wa tatu kushoto) akiwa na baadhi ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wastaifu wakielekea kwenye eneo litakalofungwa mashine za kuzalisha umeme (Power house) ili kuangalia maendeleo ya kazi hiyo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Bw. Kheri Abdul Mahimbali (wa kwanza kulia) akizungumza na baadhi ya watendaji walioshiriki ziara ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wastaifu katika mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere.





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mafuta ya Taifa ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ENOC LLC, Bw. Saif Al Falasi aliyeambatana na ujumbe wake Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 28 Januari, 2023.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Nishati tarehe 27 Januari, 2023 ilisaini Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Understanding) na Kampuni hiyo ya ENOC LLC kuhusu Ujenzi wa Kitovu cha Mafuta (Fuel Hub) hapa nchini.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mafuta ya Taifa ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ENOC LLC, Bw. Saif Al Falasi mara baada ya mazungumzo Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 28 Januari, 2023. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Nishati tarehe 27 Januari, 2023 walisaini Mkataba wa makubaliano (Memorandum of Understanding) na Kampuni hiyo ya ENOC LLC kuhusu Ujenzi wa Kitovu cha Mafuta (Fuel Hub) hapa nchini.

## SERIKALI KUBADILI UTARATIBU WA KUTOA KAZI KWA WAKANDARASI WA MIRADI YA UMEME VIJIJINI



*Waziri wa Nishati, Mhe. Januari Makamba akizungumza na Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini katika kikao maalum kilichofanyika Dar es Salaam, Januari 24, 2023.*

### **Veronica Simba – Dar es Salaam.**

**W**aziri wa Nishati, Mheshimiwa Januari Makamba amesema Serikali iko katika mchakato wa kubadilisha utaratibu mzima wa kutoa kazi kwa Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini kwa kuzingatia zaidi watakaokidhi vigezo vya utekelezaji miradi kwa wakati na viwango.

Aliysema hayo Januari 24, 2023 jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini.

Alisema Serikali imewekeza fedha nyingi katika utekelezaji wa miradi hiyo hivyo

haiwezi kukubali kuona wananchi wakiendelea kulalamika kutoptaka na kucheleweshwa kwa miradi husika.

"Tuko katika mchakato wa kubadilisha kabisa namna nzima tunawapa kazi, namna nzima tunatathmini hizi kazi na mwishowe hatima yenu kama Wakandarasi wa miradi ya REA."

Akieleza zaidi, Waziri amesema Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) itafuata taratibu zote na kuhakikisha inawaengua ambao wanababisha malalamiko.

Aidha, alisisitiza kuwa kwa wale ambao wana utekelezaji duni zaidi na hawabadiliki, Serikali siyo tu kwamba itawachukulia hatua za kimkataba lakini pia itawashtaki kwenye Bodi ya Usajili wa

Wahandisi (Contractors Registration Board) ili waondolewe katika orodha ya Wakandarasi wa Tanzania.

"Haiwezekani wewe umepewa kazi unaendelea nayo, labda ulipaswa kuwa umefikia asilimia 90 lakini uko asilimia 40 na mwenzako kafikia asilimia 90 inayotakiwa halafu mnaenda kwenye ushindani huku mkiwa mmepewa nafasi sawa ya kupata kazi nyingine," amefafanua.

Waziri Makamba alisisitiza kuwa ni kwa sababu hiyo, utaratibu unababilishwa na kwamba Mkandarasi akipewa kipande kidogo cha kazi, akikamilisha atapewa kipande kingine na siyo vinginevyo.

Kufuatia kusuasua kwa baadhi ya wakandarasi katika utekelezaji wa

miradi, Waziri Makamba alitoa muda wa miezi miwili kuanzia sasa ili waitumie kurekebisha dosari na mapungufu yao ili wafikie kiwango kinachotakiwa.

"Kama ulikuwa umesuasua, uko nafasi za chini au ya mwisho, tumia muda huo wa miezi miwili kuchakarika ili ufike kwenye nafasi inayotakiwa," alielekeza.

Akifafanua zaidi, alisema baada ya mwezi mmoja tangu kutolewa kwa agizo, Serikali itafanya tathmini ili kuanza kubaini waliozingatia maelekezo na kufanya mabadiliko na baada ya miezi miwili wale watakaokuwa na utekelezaji duni watakuwa wamefungua wigo wa kutoka nje.

Pamoja na kutoa maelekezo hayo, Waziri aliweka bayana kuwa



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali akizungumza wakati wa kikao maalum cha Waziri wa Nishati, Mhe. Januari Makamba na Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini kilichofanyika Dar es Salaam, Januari 24, 2023.*

## SERIKALI KUBADILI UTARATIBU WA KUTOA KAZI KWA WAKANDARASI WA MIRADI YA UMEME VIJIJINI



Mjumbe wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Mhandisi Styden Rwebangila akizungumza wakati wa kikao maalum cha Waziri wa Nishati, Mhe. Januari Makamba na Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini kilichofanyika Dar es Salaam, Januari 24, 2023.

lengo la Serikali ni kuwapa fursa wakandarasi wazawa lakini akatoa angalizo endapo wakashindwa kutimiza vigezo, basi Serikali haitasita kuwapatia kazi hizo Wakandarasi wa kimataifa waliothibitika kufanya kazi nzuri katika nchi mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Waziri aliwaagiza Wakandarasi wote wenyewe utekelezaji duni kuwasilisha REA, Mpango wa namna ya kushughulikia ucheleweshaji miradi uliotokea (Delay Recovery Program) ndani ya siku saba tangu kutolewa kwa maagizo husika.

Akizungumzia mikakati zaidi iliyochukuliwa na Wizara kwa kushirikiana na REA katika kuhakikisha miradi ya umeme vijijini inatekelezwa kwa wakati,

Waziri Makamba alisema mchakato wa kuajiri vijana 136 kwa kazi ya kusimamia miradi ya REA nchi nzima uko katika hatua za mwisho kwani usaili umekwishafanyika na hivi karibuni wataanza kazi.

Aidha, alibainisha kuwa, kunaandaliiwa Jukwaa maalum kupitia tovuti (Website Portal) litakalotumika kuhuishwa taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ili kila mwananchi atakayeingia humo aweze kuona kwa uwazi hali halisi, wapi kunaendelea vizuri na wapi kunasusua ili waweze kuhoji.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Mkuu wa REA Mhandisi Hassan Saidy aliwakaribisha Wakandarasi wenyewe

kuhitaji mazungumzo au msaada wowote kutoka REA, hususan waliokamilisha taratibu na wakawa na changamoto za kutokulipwa kwa wakati, wafike ofisini kwake, ambapo aliahidi kuzitatuwa.

"Niwahakikishie tu kwamba sisi REA tumeshakubaliana na kuweka mikakati

ya dhati kwamba hatutachelewesa malipo kwa Wakandarasi kwani tunatambua umuhimu wa miradi hiyo kwa wananchi," alisisitiza Mhandisi Saidy.

Akizungumza kwa niaba ya Wajumbe wenzake wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB), Mhandisi Styden Rwebangira alisema ni faida zaidi kwa



Sehemu ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe. Januari Makamba alipokuwa akizungumza nao katika kikao maalum kujadili utekelezaji wa miradi hiyo. Kikao hicho kilifanyika jijini Dar es Salaam, Januari 24, 2023.

## SERIKALI KUBADILI UTARATIBU WA KUTOA KAZI KWA WAKANDARASI WA MIRADI YA UMEME VIJIJINI



Waziri wa Nishati, Mhe. Januari Makamba akiwa katika picha ya pamoja na Wakandarasi walioshika nafasi nne za juu katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini. Tukio hilo liliifanyika wakati wa kikao cha Waziri na Wakandarasi jijini Dar es Salaam, Januari 24, 2023.

Wakandarasi kupata fursa ya kuelezwu bayana mipango na hatua ambazo Serikali inakwenda kuzichukua dhidi ya wale wenye utekelezaji hafifu.

Alisema Serikali ingeweza isiweke bayana na kuchukua hatua kimyakimya hali ambayo ingewaathiri kwani wasingepata fursa ya kujirekebisha kama wanayopewa sasa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Namis Corporate, Mhandisi Thomas Uiso, akizungumza kwa niaba ya Wakandarasi wote wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini, alisema wamepokea maelekezo ya Mheshimiwa Waziri na

watayafanyia kazi maana wanataka kuendelea kudumu katika kazi hizo. "Nikuhalikishie Mheshimiwa waziri, katika wale watano wa juu kwa utekelezaji mzuri wa miradi, baada ya miezi miwili idadi itabadilika kabisa," alisisitiza.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, Mkurugenzi wa Huduma za Ufundu kutoka REA, Mhandisi Jones Olotu aliitaja kampuni ya M/s STEG International Limited kufanya kazi nzuri kwani Mkandarasi huyo amekamilisha ujenzi wa miundombinu yote ya mradi kwa asilimia 100 kabla ya muda wa mradi

kukamilika. Alisema kazi aliyokamilisha Mkandarasi huyo ni kwa fungu (lot) 30 katika wilaya za Meatu na Maswa mkoani Simiyu na fungu 18 katika Wilaya ya Morogoro Vijijini mkoani Morogoro.

Mhandisi Olotu aliongeza kuwa ili kuhakikisha wananchi wengi wanaunganishwa na huduma ya umeme, Wakala umeongeza wigo wa njia za msongo mdogo (LV lines) kwa kilomita 2 pamoja na wateja 42 kwa kila kijiji.

Mkandarasi M/s STEG na wengine wawili kutoka kampuni za SAGEM COM Company Ltd na China Railway &

Electrification Bureau wamepewa mkono wa pongezi na Mheshimiwa Waziri na watapatiwa zawadi maalum kutoka REA kutambua utendaji kazi wao mzuri katika kutekeleza miradi ya umeme vijijini.

Wakandarasi hao wameongoza kwa kushika nafasi nne za juu katika utekelezaji miradi.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, Kamishna wa Umeme na Nishati na Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga, Wajumbe wa Bodii ya Nishati Vijijini, Wataalamu kutoka REA, TANESCO na Wizarani.

## MILANGO YA UWEKEZAJI NISHATI IPO WAZI - MAKAMBA



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza na wadau wa sekta ya Nishati  
Februari 01, 2023 mkoani Dar es Salaam.

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amesema Tanzania imeweka milango wazi kwenye uwekezaji wa Sekta ya Nishati kutohana na uwepo wa mahitaji makubwa ya nishati nchini.

Waziri Makamba ameyasema hayo mkoani Dar es Salaam katika mkutano wa Wadau wa Nishati, Wawekezaji, Makampuni ya Nishati kutoka Nje, Mabalozi wa Nchi mbalimbali ambao unaangazia hali ya nishati sambamba na

maendeleo yaliyofikiwa. "Tumewakaribisha wawekezaji, tupo tayari kuhakikisha uwekezaji wao unakuwa wenye tija zaidi, hata hivyo serikali ipo tayari kuweka nguvu kwa sekta binafsi kwa maslahi mapana ya kupiga hatua za

kimaendeleo nchini Tanzania". Amesitisita Waziri Makamba amesema "Kwanini Tanzania?, Kwanini sasa? Tanzania ni mahali sahihi penye amani katika kufanya uwekezaji, hivyo tunawakaribisha Wawekezaji wenye tija kuwekeza kwenye Sekta ya Nishati Nchini"

Kwa upande wao Washiriki katika Mkutano huo wamepongeza juhudzi za Serikali katika Sekta ya Nishati kwa kufungua wigo wa uwekezaji sambamba na kutatua changamoto zinazoikabili Sekta hiyo ikiwemo urasimu.

Mkutano umeandaliwa na EnergyNet kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati, EWURA, TPDC na TANESCO.



Wadau wa Nishati kutoka ndani na nje ya nchi wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba wakati wa Mkutano wa Tatu wa Wadau hao uliofanyika mkoani Dar es Salaam.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (kushoto) akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipotoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma. Kushoto kwake Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Styden Rwebangila.

## MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE WAFIKIA ASILIMIA 80.2

### **Na Teresia Mhagama - Dodoma**

**N**aibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, amesema kuwa utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 2,115 umefikia asilimia 80.2.

Naibu Waziri Byabato aliyasema hayo tarehe 17 Januari, 2023, wakati Wizara ya Nishati ikitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini

jijini Dodoma.

"Kwa sasa utekelezaji wa mradi unaenda kwa kasi ambapo hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2022 umefikia asilimia 80.22, aidha mnamo tarehe 22 Desemba, 2022 zoezi la kuanza kujaza maji katika bwawa la JNHPP lilifanyika kwa kufunga mageti ya njia ya mchepusho." Alisema Byabato

Kuhusu kazi ya ujazaji maji katika Bwawa la JNHPP amesema kuwa, hadi kufikia tarehe 16 Januari, 2023 kimo cha maji cha Bwawa kilifikia mita 112.48 kutoka usawa wa bahari kutokea kimo cha mita 74 tarehe 22

Desemba 2022.

Naibu Waziri aliongeza kuwa, utekelezaji wa mradi wa JNHPP unaenda sanjari na utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400 kutoka eneo la mradi hadi Chalinze mkoani Pwani na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambapo kwa ujumla miradi hiyo inaendelea kutekelezwa kwa kasi.

Kuhusu malipo kwa mkandarasi wa mradi huo alisema kuwa, tayari Serikali imeshalipa asilimia 74.7 ya malipo hayo ambapo gharama za mradi huo ni shilingi Trilioni 6.5.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Dunstan Kitandula amepongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huo ikiwemo hatua ya kuanza kujaza maji kwenye bwawa hilo. Aidha alisisitiza mradi huo kuendelea kutekelezwa kwa kasi ili asilimia za utekelezaji zilizobaki zikamilike kwa wakati.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Styden Rwebangila pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

# MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE WAFIKIA ASILIMIA 80.2



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula (mbele, kushoto) akizungumza baada ya Wizara ya Nishati kutoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kwa Wajumbe wa Kamati hiyo jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (mbele, kushoto) akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma. Kushoto kwake Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Styden Rwebangila.



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Mhe. Isaac Njenga (kulia) wakizungumza kuhusu ushirikiano wa Tanzania na Kenya katika Sekta ya Gesi na Umeme katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma.*

## Tanzania na Kenya zajadili ushirikiano Sekta ya Umeme na Gesi

### **Na Teresia Mhagama**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba pamoja na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Mhe. Isaac Njenga wamekutana na kufanya mazungumzo kuhusu ushirikiano wa Tanzania na Kenya katika Sekta ya Umeme na Gesi.

Mazungumzo hayo yalifanyika tarehe 18 Januari, 2023 jijini Dodoma ambapo viongozi hao walizungumzia ushirikiano katika kuendeleza nishati ya Jotoardhi, Jua, Upepo pamoja na mradi ya usafirishaji Gesi, usafirishaji umeme na



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akiwa na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Mhe. Isaac Njenga (kulia) mara baada ya kumaliza mazungumzo kati yao kuhusu ushirikiano wa Tanzania na Kenya katika Sekta ya Gesi na Umeme katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma.*

usambazaji umeme vijiini.

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba alimueleza Balozi Njenga kuwa, Tanzania ipo tayari kuendeleza ushirikiano na Kenya katika Sekta ya Gesi na Umeme kwani nchi hizo tayari zina ushirikiano kwenye sekta mbalimbali ikiwemo miundombinu ya barabara na anga.

Kuhusu mradi wa usafirishaji Gesi kutoka Tanzania kwenda Kenya, alisema kuwa mradi huo ni wa kipaumbele kwa viongozi Wakuu wa nchi hizo mbili na kwamba tayari timu za majadilino kutoka Kenya na Tanzania zimeshaundwa na zinaendelea na kazi ya kuandaa nyaraka mbalimbali zitakazowezesha mradi huo kusonga mbele.

Aidha, kuhusu ushirikiano kwenye Jotoardhi alisema

# Tanzania na Kenya zjadili ushirikiano

## Sekta ya Umeme na Gesi



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akimsikiliza Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Mhe. Isaac Njenga (kulia) mara baada ya kufika katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma ili kuzungumza masuala yanayohusu ushirikiano wa Tanzania na Kenya katika Sekta ya Gesi na Umeme.*

kuwa, Tanzania imeshaanza kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza vyanzo hivyo ikiwemo za upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi na kwamba mtambo wa uchorongaji visima vya jotoardhi kwa ajili ya kuendeleza Jotoardhi unatarajiwa kuwasili nchini mwezi wa Pili mwaka 2023.

Vilevile, alisema Tanzania ipo tayari kushirikiana na Kenya katika kuendeleza vyanzo vya umeme jadidifu vikiwemo Jua na Upopo.

Kuhusu ushirikiano katika miradi ya umeme vijijini, alisema kuwa, ushirikiano huo ni muhimu kwani Tanzania na Kenya zitaweza

kubadilishana uzoefu, na hivyo kuweza kufikisha huduma ya umeme vijijini kwa ufanisi zaidi.

Kwa upande wake, Balozi wa Kenya nchini

Tanzania, alimueleza Waziri wa Nishati kuhusu nia ya nchi hiyo kushirikiana na Tanzania katika uendelezaji wa nishati ya Jotoardhi kwani Tanzania ina vyanzo vya kutosha kuweza kuzalisha umeme kwa kutumia Jotoardhi.

Alisema kuwa, Kenya tayari imeshapiga hatua katika uendelezaji wa Jotoardhi kwani kwa sasa wanazalisha takribani megawati 986 za umeme kwa kutumia nishati hiyo ambayo ni asilimia 46 ya umeme wote unaozalishwa nchini Kenya.

Aidha, Mhe. Balozi Isaac Njenga alimueleza Waziri wa Nishati kuhusu utayari wa Kenya katika kutekeleza makubaliano

ya ushirikiano yaliyoingiwa kati ya nchi hizo mbili kwenye miradi wa usafirishaji gesi kutoka Tanzania na miradi ya usafirishaji wa umeme kwa msongo wa KV 400 ambayo itawezesha nchi hizo mbili kuweza kuuziana umeme.

Vilevile, alimueleza Waziri wa Nishati kuhusu Kenya na Tanzania kushirikiana katika miradi ya usambazaji umeme vijijini hali itakayowezesha kila nchi kujifunza mbinu za mafanikio ya usambazaji umeme vijijini.

Kwa upande wa Serikali ya Tanzania, kikao hicho kilihudhuriwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga na Kaimu Kamishna Msaidizi wa Gesi, Mhandisi Joyce Kisamo



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akizungumza na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Mhe. Isaac Njenga (kulia) kuhusu masuala yanayohusu ushirikiano wa Tanzania na Kenya katika Sekta ya Gesi na Umeme katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma. Wengine Katika picha ni Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Eng. Innocent Luoga na Kaimu Kamishna Msaidizi wa Gesi, Eng. Joyce Kisamo.*

# Uzalishaji wa Umeme na Gesi Asilia waongezeka



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha mwezi Julai-Desemba, 2022 jijini Dodoma.

## **Na Teresia Mhagama - Dodoma**

meelezwa kuwa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyoungwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umeongezeka na kufikia megawati 1,777.05 mwezi Desemba 2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.87, ikilinganishwa na megawati 1,694.55 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Septemba 2022.

Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2022 jumla ya futi za ujazo milioni 38,172 za Gesi Asilia zilizalishwa katika vitalu vya Songsongo na

Mnazi Bay ambapo uzalishaji wa Gesi asilia umeongezeka kwa asilimia 27 ikilinganishwa na kipindi Julai-Desemba, mwaka 2021 ambapo futi za ujazo 29,996 zilizalishwa.

Hayo yalielezwa tarehe 20 Januari, 2023 jijini Dodoma wakati Wizara ya Nishati ikiongozwa na Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba ilipowasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha mwezi Julai-Desemba, 2022.

Waziri wa Nishati, alisema kuwa, ongezeko la uwezo wa mitambo hiyo ya kuzalisha umeme

iliyoungwa katika mfumo wa gridi limetokana kuingizwa katika Gridi ya Taifa megawati 90 za umeme zinazozalishwa katika Kituo cha Kinyerezi I Extension.

Aidha, alisema kuwa, uwezo wa kuzalisha umeme kwa mitambo ambayo haijaunganishwa katika Gridi ya Taifa umefikia megawati 39.302 na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini kufikia megawati 1,816.352 ikilinganishwa na megawati 1,733.38 zilizokuwepo mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.89.

Kuhusu kuongezeka kwa uzalishaji wa

Gesi asilia alisema kuwa "ongezeko hili limetokana na ufungaji wa kompresa tatu katika Kitalu cha Songsongo ambazo zimeongeza mgandamizo na msukumo wa Gesi kutoka kisimani na sasa wastani wa futi za ujazo milioni 240 zinazalishwa kwa siku kutoka katika vitalu vya Songsongo na Mnazi Bay.

Gesi hiyo inayozalishwa, inatumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani, kwenye Taasisi, magari na uzalishaji wa wastani wa asilimia 62 ya umeme wa Gridi ya Taifa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati pamoja na kuishukuru Wizara kwa kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti yake, alitoa maelekezo mbalimbali yatakayosaidia kutekeleza bajeti hiyo kwa ufanisi zaidi.

Katika kikao hicho na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Wizara pia ilieleza utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoendelea kutekeleza ikiwemo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya Gesi na Umeme mijini na vijiji.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha mwezi Julai-Desemba, 2022. Wa kwanza kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato na wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara.



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijiini (REA), Mhandisi Hassan Saidy akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha mwezi Julai-Desemba, 2022. Wa Pili kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati. Mhe. January Makamba na wa kwanza kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Nishati, Petro Lyatuu (aliyesimama) akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwezi Julai-Desemba, 2022 kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma. Wengine katika picha ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini ya Wizara.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandu akizungumza mara baada ya Wizara ya Nishati kuwasilisha kwa Kamati hiyo utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwezi Julai-Desemba, 2022 jijini Dodoma.



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipotua taarifa ya mwenendo wa upatikanaji wa mafuta nchini kwa wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Jijini Dodoma.

## SERIKALI KUENDELEA KUBORESHA MAGHALA YA KUHIFADHI MAFUTA-MAKAMBA

### Na.Godfrey Mwemezi-Dodoma

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amesema kuwa serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kupata wawekezaji watakaojenga Ghala kuu la kupoolea mafuta kwa pamoja ili kuwezesha nchi kuwa na uhakika zaidi wa upatikanaji wa mafuta.

Makamba aliyasema hayo tarehe 19 Januari, 2023, wakati Wizara ya Nishati ikitoa taarifa ya mwenendo wa upatikanaji wa mafuta nchini kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

Alisema kuwa, uwepo wa ghalo hilo utawezesha shehena kubwa za mafuta kupakuliwa kwa haraka na hivyo kupunguza gharama za uagizaji, ucheleweshaji wa meli na kuendelea kuleta unafuu wa bei za bidhaa za mafuta nchini.

"Serikali imeanza kutumia ghalo la TIPER kwa ajili ya kupoolea mafuta ya dizeli yanayoingia nchini kuititia bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza muda wa kupoolea mafuta hayo kutoka katika meli. Alisema Makamba

Alieleza kuwa, Serikali itajenga pia gati kubwa la kupoolea mafuta ya petroli na kuboresha gati kubwa la kupoolea

mafuta ya dizeli. Gati hizo zitaakisi mahitaji ya sasa na miaka ya baadaye ikiwemo kujenga gati kubwa lenye mabomba ya kupakua mafuta na kuwezesha kupoolea meli kubwa zenye uwezo wa kubeba tani 100,000 za petroli, tani 200,000 za dizeli na tani 40,000,000 za gesi ya mitungi (LPG).

Alongeza kuwa, Serikali itaendelea kufuatilia mwenendo wa bei ya mafuta katika soko la dunia na gharama za uagizaji ili kuweza kuchukua hatua stahiki zitakazopunguza makali ya bei kwa wananchi na katika uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Dunstan Kitandula

aliipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali zinazochuliwa katika shughuli za upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na unafuu wa bei za bidhaa za mafuta katika soko la ndani.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha.Felchesmi Mramba, pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati, Mamlaka ya Udhhibit wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kampuni ya kuhifadhi mafuta ya TIPER pamoja na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula (wa kwanza kushoto), akiwasikiliza wajumbe wakati Wizara ya Nishati ilipota taarifa ya mwenendo wa upatikanaji wa mafuta nchini kwa wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kushoto), akiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba (wa pili kulia), wakifuatilia hoja mbalimbali za Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakati Wizara ya Nishati ilipota taarifa ya mwenendo wa upatikanaji wa mafuta nchini kwa wajumbe hao, bungeni Jijini Dodoma.

## MIUNDOMBINU YA UMEME NCHINI IMEIMARIKA



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (kushoto) akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipotoa taarifa ya hali ya Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa umeme nchini kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

### **Na.Timotheo Mathayo-** **Dodoma**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amesema kuwa hali ya miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini imeendelea kuimarika na kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa wateja.

Makamba aliyasema hayo tarehe 18 Januari, 2023, wakati Wizara ya Nishati ikitoa taarifa ya hali ya umeme nchini kwa wajumbe wa Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

Makamba alisema kuwa, Serikali

imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya Umeme na kujenga miundombinu mipywa ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya shilingi bilioni 711.56 zitatumika kwa kazi husika zikijumuisha shilingi bilioni 400 za kuimarisha Gridi.

"Kupitia miundombinu hiyo, TANESCO imeweza kuunganishia wateja wapya 331,034 ndani ya miezi sita kuanzia Julai, 2022 hadi Desemba, 2022 sawa na asilimia 166 ya lengo

**Kikao hicho kilihudhuriwa pia Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadiifu, Mha. Innocent Luoga pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na Wakala wa Nishati Vijiji (REA).**

la kuunganisha wateja wapya 200,000 katika kipindi hicho. Alisema Makamba

Alisema kuwa, kuvuka kwa lengo hilo kumetokana na kuanzishwa kwa mfumo mpya wa maombi ya umeme wa Nikonekt pamoja na utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini na kufanikisha kufikia wateja 4,173,130 ikilinganishwa na wateja 3,655,534 waliokuwepo kufikia mwezi Januari, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 13.47.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Dunstan Kitandula alipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazozichukua ili kuhakikisha hali ya miundombinu ya kusambaza na kusafirisha umeme nchini inaendelea kuimarika pamoja na uzalishaji wa umeme.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadiifu, Mha. Innocent Luoga pamoja na watendaji wengine kutoka Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na Wakala wa Nishati Vijiji (REA).



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Dunstan Kitandula (wa kwanza kushoto), akizungumza wakati Wizara ya Nishati ilipotoa taarifa ya hali ya Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa umeme nchini kwa wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa kwanza kushoto) akifuatilia hoja mbalimbali za wajumbe, wakati Wizara ya Nishati ilipotoa taarifa ya hali ya Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa umeme nchini kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini jijini Dodoma.

# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*

Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au

Wasiliana nasikwa **simu namba:** +255-26-2322018

**Nukushi:** +255-26-2320148